
## MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024 KWA MKOA WA KUSINI UNGUJA
**Umetolewa: 22/08/2024**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2024; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Kusini Unguja na wilaya zake:

**(I) Ngazi ya Mkoa**




**Kielelezo 1: (a)** Mwelekeo wa msimu wa Vuli, 2024 kwa kisiwa cha Unguja. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Vuli katika sehemu mbalimbali za kisiwa cha Unguja. **Angalizo**: Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

### Dondoo

*(i). Kwa ujumla mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini Unguja.*
*(ii). Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na tatu ya mwezi Oktoba, 2024.*
*(iii). Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.*
*(iv). Vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi vinatarajiwa katika msimu huu wa Vuli.*

**Mvua za msimu wa Vuli, 2024**

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini Unguja. Msimu huu unatarajiwa kuanza kwa kusuasua na kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.


***Angalizo:***
*Ingawa maeneo mengi yanatarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani, izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo machache.*

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024 KWA WILAYA YA KATI
**Umetolewa: 22/08/2024**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2024 athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kati.




Mwelekeo wa mvua za Vuli Oktoba-Disemba, 2024 kwa Wilaya ya Kati, Unguja.

### Dondoo muhimu

(i). *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kati.*
(ii). *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na tatu ya mwezi Oktoba, 2024.*
(iii). *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.*
(iv). *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2024 kwa wilaya ya Kati

**Zitaanza:** Wiki ya pili na tatu ya mwezi Oktoba, 2024.

**Zitaisha:** Wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba - Disemba kwa wilaya ya Kati ni kati ya milimita 180 hadi 290.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2024.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea kwa vipindi virefu vya ukavu katika msimu huu wa Vuli, 2024.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i). Upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na matunda yakiwemo mpunga, migomba, mahindi, mtama, karafuu, nazi na michungwa.
(ii). Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.
(iii). Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.
(iv). Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kupungua.

#### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
(ii). Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
(iii). Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**


*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

(II) Ngazi ya Wilaya

## MWELEKEO WA MVUA ZA VULI (OKTOBA – DISEMBA), 2024 KWA WILAYA YA KUSINI
**Umetolewa: 22/08/2024**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2024 athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kusini.




Mwelekeo wa mvua za Vuli Oktoba-Disemba, 2024 kwa Wilaya ya Kusini, Unguja.

### Dondoo muhimu

(i). *Mvua za chini ya wastani hadi wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kusini.*
(ii). *Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili na tatu ya mwezi Oktoba, 2024.*
(iii). *Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.*
(iv). *Wakulima na wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji na uzalishaji wa mazao ili kukabiliana na upungufu wa mvua.*

### Mvua za msimu wa Vuli, 2024 kwa wilaya ya Kusini

**Zitaanza:** Wiki ya pili na tatu ya mwezi Oktoba, 2024.

**Zitaisha:** Wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2024.

**Kiasi cha mvua zinazotarajiwa:** Mvua zinatarajiwa kuwa chini ya wastani hadi wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Oktoba - Disemba kwa wilaya ya Kusini ni kati ya milimita 180 hadi 240.

**Kiwango cha juu cha mvua:** Kinatarajiwa katika mwezi Disemba, 2024.

**Vipindi vya ukavu:** Upo uwezekano wa kutokea kwa vipindi virefu vya ukavu katika msimu huu wa Vuli, 2024.

**Ulinganifu:** Mvua zinatarajiwa kuwa chache na zenye mtawanyiko hafifu katika maeneo mengi ukilinganisha na Vuli iliyopita.

### Angalizo:

- **Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.**

- **Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

### Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi

#### Matokeo

(i). Upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo katika maeneo mengi unaweza kuathiri uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na matunda yakiwemo mpunga, migomba, mahindi, mtama, karafuu, nazi na michungwa.
(ii). Magonjwa ya mifugo na wadudu waharibifu wa mazao hasa wakati wa msimu wa mvua yanaweza kujitokeza.
(iii). Upungufu wa mvua unaweza kuathiri upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.
(iv). Uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya baharini unatarajiwa kupungua.

#### Ushauri

(i). Wakulima wanashauriwa kupanda mbegu bora za muda mfupi zinazoendana na urefu wa msimu.
(ii). Wakulima wanashauriwa kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua.
(iii). Wafugaji wanashauriwa kufuata njia bora za ufugaji ikiwemo kupanda malisho na uhifadhi.

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: **www.meteo.go.tz**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727N – 01/2023*